



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

HAFLA YA PILI YA UTOAJI VYETI KWA MADEREVA WALIOTHIBITISHWA

*Dar es Salaam,
Tarehe 24 Mei, 2024.*

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la Kusajili Wahudumu na Kuthibitisha Madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara.

Katika kutekeleza jukumu hilo, tarehe 01 Disemba, 2020 LATRA ilianza kusajili madereva husika na tarehe 01 Juni, 2022 walianza kutahiniwa kwa lengo la kuthibitishwa. Aidha, Julai 01, 2023 jumla ya madereva **999** walitunukiwa vyeti vya uthibitisho vya LATRA baada ya kufanya mtihani na kufaulu.

Mamlaka inawatangazia madereva wote waliofanya mtihani na kufaulu kuanzia tarehe 1 Juni, 2023 hadi tarehe 31 Machi, 2024 kuwa imeandaa hafla ya pili ya kuwatunuku vyeti ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Hafla hiyo itafanyika Jumanne tarehe 04 Juni, 2024 Ukumbi wa Mikutano wa Arnaoutoglou Jijini Dar es Salaam kuanzia saa 4 (nne) kamili asubuhi. Madereva watakaohudhuria hafla hiyo wanaombwa kuthibitisha ushiriki kwa kutuma ujumbe mfupi wa maandishi wenye jina kamili kama lilivyo katika Kitambulisho cha Taifa kwenda simu namba **0734 220 006** au **0738 418 430** kabla ya tarehe 2 Juni, 2024.

Salum Pazy
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano